Mradi wa WOLTS Tanzania

Muhtasari wa Ripoti--Naisinyai

Septemba 2017

Daley, E., Lanz, K., Mhinda, A., Driscoll, Z., Ndakaru, J., Grabham, J. na Kereri, E.

mokoro

HakiMadini

Muhtasari huu unawakilisha matokeo ya jumla ya utafiti uliofanywa chini ya mradi wa WOLTS Tanzania—Ripoti ya Kijiji cha Naisinyai, Septemba 2017, inapatikana kwenye tovuti hii www.mokoro.co.uk/wolts.

Maandishi © Timu ya WOLTS. Picha zote © Timu ya WOLTS.

Utafiti na Mbinu za mradi wa WOLTS

Ni mradi wa mpango mkakati wa muda mrefu wa utafiti unaofanywa na Mokoro kwa kushirikiana na HakiMadini "kutafiti changamoto za usalama wa umiliki wa ardhi kwa wanawake nchini Tanzania". Mokoro kwa kushirikiana na HakiMadini Tanzania, wamekuwa wakitafiti hali ya usalama wa umiliki wa ardhi kwa wanawake wa jamii za kifugaji zinazoathiriwa na uwekezaji wa uchimbaji madini kupitia njia shirikishi za utafiti ili kubaini changamoto/vikwazo mbalimbali vya haki za ardhi kwa wanawake na makundi maalumu. Mradi wa WOLTS unalenga kutathmini njia sahihi za kuboresha usawa wa kijinsia katika umiliki na usimamizi wa haki za ardhi ili kulinda haki za umiliki wa ardhi kwa makundi maalumu dhidi ya vikwazo/changamoto katika jamii husika pamoja na kusaidia jamii kwa ujumla kuhimili changamoto juu ya umiliki wa ardhi na maliasili zao(angalia tovuti yetu www.mokoro.co.uk/wolts/).

Muhtasari huu unashirikisha matokeo yetu yatokanayo na utafiti wetu uliofanyika katika Kijiji cha Naisinyai kati ya Juni 2016 na Februari 2017, ikiwa ni pamoja na ziara za awali, utafiti wa awali na utafiti shirikishi. Tunawashukuru watu wote wa kijiji cha Naisinyai kwa ushiriki na ukarimu wao wakati wote wa utafiti na msaada mkubwa uliotolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro.

Utafiti wa awali ulifanyika Agosti 2016 kwa kuhusisha asilimia kumi (10%) ya kaya ndani ya kijiji kizima cha Naisinyai. Utafiti ulihusisha kaya 125, ambapo kaya 103 kati ya hizo zilichaguliwa bila kuzingatia vigezo maalumu na kaya 22 zilikuwa kaya za ziada zinazoongozwa na wanawake. Hivyo 82% ya jumla ya sampuli ya utafiti ilichaguliwa bila kuzingatia vigezo maalumu (ikihusisha kaya 97 zinazoongozwa na wanaume na sita zinazoongozwa na wanawake) wakati 18% ilikusudiwa ziwe kaya zinazoongozwa na wanawake (kaya 22). Hili lilifanyika ili kuongeza idadi ya kaya zinazoongozwa na wanawake katika utafiti ili kuibua masuala muhimu ya kijinsia na makundi maalumu. Taarifa kutoka kaya 22 zinazoongozwa na wanawake zimehusishwa ili kulinganisha matokeo na kaya zinazoongozwa na wanaume na siyo matokeo ya jumla ya utafiti.

Awamu ya utafiti shirikishi ilikuwa Februari 2017 na ilihusisha majadiliano ya makundi lengwa 13 na mahojiano ya watu binafsi 12 na kufanya jumla ya watu 104. Makundi tofauti ya kijamii na watu binafsi walichaguliwa mahususi kwa majadiliano na mahojiano ili kuakisi tabia na masuala yanayodhaniwa kuwa muhimu kuchunguzwa zaidi baada ya uchambuzi wa taarifa za matokeo wa utafiti wa awali (Mfano: wajane, wachimbaji, walio kwenye ndoa ya mke mmoja, walio kwenye ndoa ya wake wengi, n.k). Majadiliano ya makundi lengwa yaliundwa kwa kuzingatia viwango vya mazoezi shirikishi (yakihusisha maliasili na misimu ya kuhamahama, uchambuzi wa kazi za msimu, uchambuzi wa wadau na ushirikiano baina ya taasisi mbalimbali). Mahojiano ya wasifu yaliongozwa na muundo wa maswali ambayo yalifumwa kutokana na hali za wahojiwa binafsi ili kusaidia kufahamu maisha ya watu na namna ambavyo mahusiano ya kijinsia na upatikanaji wa rasilimali mbalimbali ulivyobadilika tangu utotoni. Majadiliano ya makundi lengwa yote na mahojiano ya watu binafsi yalihusisha majadiliano huru pia. Utafiti wa mradi ulihusisha mahojiano na viongozi mbalimbali wa serikali za mitaa pamoja na wawakilishi kutoka baadhi ya kampuni za uchimbaji na mashirika yanayofanya kazi Naisinyai.

Eneo na idadi ya watu

Kijiji cha Naisinyai kiko katika kata ya Naisinyai wilaya ya Simanjiro, mkoa wa Manyara, kaskazini mwa Tanzania. Mji wa kiwango cha kati Mirerani, unapakana na Naisinyai kusini; Makao makuu ya wilaya ya Simanjiro yapo kilomita takribani 145 kusini mwa Naisinyai barabara ikiwa ya kawaida/vumbi (isiyo na kiwango cha lami) hadi mji mdogo wa Orkesumet. Kutoka kijiji cha Naisinyai hadi uwanja wa ndege wa nimataifa wa Kilimanjaro ni takribani kilomita 19, barabara ikiwa ya kiwango cha lami. Kutoka huko ni zaidi ya kilomita 65 magharibi hadi mji mkuu wa Arusha. Hakuna taarifa sahihi iliyopatikana kuhusiana na eneo la ardhi la Naisinyai, ingawa viongozi wa kijiji walidhani kuwa ni karibu Kilomita 30 za mraba (30 km^2). Matumizi makuu matatu ya ardhi ya kijiji ni ufugaji,

kilimo cha mazao na uchimbaji wa madini. Sehemu za Naisinyai inajumuishwa ndani ya mipaka ya Eneo tengefu la Mirerani (MCA), eneo la kilomita 7 za ardhi ambayo ndiyo pekee inayojulikana kuwa na madini ya Tanzanite ulimwenguni. Kwa mujibu wa taarifa kutoka ofisi ya madini ya kanda Arusha, mnamo Juni 1, 2016, leseni za awali za madini 732 (PMLs) zilitolewa kwa wachimbaji wadogo wa Tanzanite ndani ya eneo tengefu la Mirerani (MCA), ambapo karibu leseni 180-200 zilikuwa zinafanya kazi, na leseni moja kubwa na mbili zikiwa za uchimbaji wa kati huko Naisinyai.

Kijiji cha Naisinyai kina vitongoji vitatu; vitongoji viwili (Olshonyokie na Naisinyai kati) viko jirani na mji mdogo wa Mirerani na vina wakazi wengi zaidi na kitongoji cha tatu watu siyo wengi sana. Kitongoji hiki cha tatu (Naepo) kilikuwa katika mchakato wa kuwa kijiji kinachojitegemea. Katika kijiji cha Naisinyai, wanafamilia wanaishi pamoja kwenye kaya tofauti zilizo karibiana, na nyumba zimejengwa karibu karibu lakini pia majengo/nyumba za kisasa zilionekana. Jumla ya idadi ya watu wa kijiji kizima kama taarifa ya 9 Agosti 2016 inavyoonesha ilikuwa ni watu 8,770 na wanaoishi katika kaya 1,243.

Asilimia sita (6%) ya kaya za sampuli za wahojiwa katika utafiti wetu wa awali zilikuwa kaya zinazoongozwa na wanawake. Kwa mujibuwa wa taarifa hii, inaonesha kuwa angalau kaya 75 za Naisinyai zilikuwa zikiongozwa na wanawake wakati wa utafiti wetu. Takwimu zetu za uchunguzi pia zinaonesha kwamba asilimia 56 ya wakazi walikuwa watoto (wenye umri wa miaka 18 au chini), 4% walikuwa wazee (wenye umri wa miaka 65 au zaidi), na 40% walikuwa kwenye umri wa kufanya kazi (wenye umri wa miaka 19 hadi 64). Angalau 77% ya sampuli ya wahojiwa katika kaya zilizohojiwa wakati wa utafiti wetu walikuwa chini ya umri wa miaka 35, matokeo ambayo ni sawa na wastani wa kitaifa. Naisinyai inakaliwa zaidi na kabila moja ambalo ni wamasai, na Ukristo ndiyo dini kuu.

Historia ya hivi karibuni ya mabadiliko ya uchumi na idadi ya watu

Kumekuwa na mabadiliko makubwa katika kijiji cha Naisinyai zaidi ya miaka 50 iliyopita, hasa kutokana na uchimbaji wa madini kuanzia miaka ya 1960. Shughuli za uchimbaji wa madini zilionekana kukuwa kwa kasi zaidi ndani ya miaka 10-20 iliyopita, na kuchangia sana uharibifu mkubwa wa mazingira kama vile ukataji miti, kupungua kwa malisho na upanuzi wa makazi kutokana na uvamizi wa watu kwenye eneo hilo, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wahamiaji kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania. Mabadiliko haya yote yamefanyika wakati Naisinyai yenyewe imebadilika kutoka kuwa jamii inayotegemea ufugaji pekee na kuwa jamii inayochanganya ufugaji na kilimo.

Mabadiliko makubwa yaliyojitokeza baada ya uanzishwaji wa vijiji mwaka wa 1974 yalikuwa ya kijamii na katika matumizi ya ardhi, kwa kuwa mabadiliko hayo yalichochewa zaidi kwa kuanzishwa kwa elimu ya msingi (UPE) mwaka 1977, na kisha kilimo cha mazao kuongezeka. Inaonekana kuwepo na ongezeko kubwa la kilimo cha mazao katika kipindi cha miaka 10 iliyopita na kuanzishwa kwa mashamba mengi makubwa ambayo yalipelekea Mto Kikuletwa kutumika kwa kilimo cha kumwagilia na ikapelekea mto huo kukauka kabisa na hivyo kilimo hicho cha umwagiliaji hakikuwa endelevu. Mabadiliko mengine baada ya uanzishwaji wa vijiji ilikuwa udhibiti mkubwa wa matumizi ya ya maeneo ya malisho, wakati huo huo maeneo ya malisho ya zamani ya kijiji cha Naisinyai yaliripotiwa kutowezekana tena kutumika kwa mifugo/malisho kutokana na uchimbaji wa madini, na njia za mifugo katika maeneo ya malisho zilifungwa ili kuepusha mifugo na athari zinazoweza kutokana na uwepo wa mashimo kwenye maeneo hayo.

Maendeleo ya Jamii na mahusiano ya Kijinsia

Ndoa na hali za familia

Wakati wa utafiti wetu, ndoa nyingi zilikuwa ni za kimila ikijumuisha asilimia ndogo (54%) ya ndoa hizi kuwa ni ya mume/mke mmoja; na ndoa ya wake wengi kwa mume mmoja zikionekana zaidi kwenye familia tajiri katika baadhi ya maeneo ya kijiji. Asilimia sabini na tisa (79%) ya kaya

zinazoongozwa na wanawake ni wajane, 145 walikuwa kwenye ndoa za wake wengi kwa mume mmoja na waume zao waliripotiwa wakati wa sensa kuwa ni wakuu wa kaya wa mke mwingine, na kaya moja inayoongozwa na mwanamke ilitengwa. Inadhaniwa kuwa inawezekana kutokana na kile kilichoelzwa kuwa baadhi ya wanaume wako kwenye ndoa ya wake wengi na hivyo wanawake hao walikua kama wametengwa, hivyo walikuwa ni kati ya wanawake walioko kwenye mazingira magumu ingawa hawakuwa tayari kutoa taarifa hizi wazi kutokana na kile kilichoelezwa kuwa kuna unyanyapaa mkubwa sana kwa wale walioachika na kupewa talaka.

Elimu

Elimu kwa ujumla ilionekana kuwa ya kiwango cha chini na watoto wa kiume (wavulana) walionekana kuwa na fursa zaidi ya kupata elimu ukilinganisha na wasichana. Hata hivyo, tulitaarifiwa kuwa wasichana wanayo fursa ya kupata elimu siku hizi ukilinganisha na ilivyokuwa zamani ambapo wasichana waliolewa wakiwa na umri mdogo sana.

Utajiri na umaskini

Makazi/nyumba katika kijiji cha Naisinyai zinatumia vifaa vya kisasa, ikiwa ni 50% ya sampuli ya wahojiwa wanaishi kwenye nyumba za matope na 10% wana nyumba za kisasa kutokana na maendeleo makubwa yaliyoletwa na uchimbaji wa madini. Pamoja na hayo, kulikuwa na utofauti mkubwa kati ya kaya zinazoongozwa na wanawake na zile zinazoongozwa na wanaume, ikiwa ni 75% ya kaya zinazoongozwa na wanawake zinaishi kwenye nyumba za matope na 48% tu ya kaya zinazoongozwa na wanaume. Kaya chache, hasa zile zinazoongozwa na wanaume wanatumia umeme au hata umeme wa jua (sola) wakati kaya zingine walikuwa wakitegemwa mwanga wa tochi za betri na taa za chemli.

Kwa kaya zote zinazoongozwa na wanaume na zinazoongozwa na wanawake katika kijiji kizima, vyanzo vya kawaida vya maji ni visima vya kina kidogo na mabomba, kwa njia ya kulipia na kugawana kwa vyanzo vyote viwili. Kulikuwa na mazingira tofauti lakini tofauti hizo ni ndogo kijinsia, kwa mfano 39% ya kaya zinazoongozwa na wanawake na 32% ya kaya zinazoongozwa na wanaume katika utafiti wetu hawakuwa na vyoo kabisa.

Kulikuwa na utofauti mkubwa wa kijinsia kwenye suala la upatikanaji wa usafiri, ingawa ilionekana kuwa sehemu kubwa ya kaya zinazoongozwa na wanawake wanamiliki baisikeli lakini watumiaji walikuwa ni wanaume wa ndani ya kaya hizo. Pikipiki ni njia kuu ya usafiri, hii ilitaarifiwa na 36% ya kaya zinazoongozwa na wanaume wakati wa utafiti wetu lakini 7% tu ya kaya zinazoongozwa na wanawake walisema hivyo.

Asilimia themanini na tatu ya sampuli ya kaya tulizohoji wakati wa utafiti wetu walikuwa wanamiliki simu, 42% walikuwa na redio na 5% wanamiliki televisheni. Kaya nyingi zinazoongozwa na wanawake hawakuwa na redio kwa wingi ukilinganisha na kaya zinazoongozwa na wanaume, lakini hakuna utofauti mkubwa wa kijinsia kwenye suala zima la kumiliki simu za mkononi, ambapo 84% ya kaya zinazoongozwa na wanaume na 75% walitaarifu kumiliki simu.

Kwa ujumla, taarifa za utafiti wetu wa awali kuhusu aina na vifaa vya ujenzi, upatikanaji wa umeme, maji, usafi na usafiri, na umiliki wa baadhi ya vitu/mali umetoa picha halisi kuhusu viwango vya umsikini katika kaya zinazoongozwa na wanawake. Hii ilidhibitishwa wakati wa utafiti shirikishi ambapo iliweka wazi/ilibaini changamoto zinazowakabili wanawake.

Vyanzo vikuu vya kipato

Karibu kila kaya inajihusisha na ufugaji wa jadi kama njia kuu ya kipato chao. Hata hivyo, mwelekeo wa kuwa na njia mbalimbali za kipato mbali na ufugaji ilitajwa kuchukuwa kasi hivi karibuni, kutokana na kile kilichoelezwa kuwa kuna ongezeko kubwa la watu, ukame wa muda mrefu na sehemu kubwa ya ardhi ya malisho kuchukuliwa na makapmuni za uchimbaji. Watu wengi walitaja

habari ya kilimo cha mazao kuwa muhimu sana, biashara za madini na biashara nyingine ndogondogo kwa ajili ya ustawi wa jamii kwa ujumla.

Hata hivyo, viwango vya kujihusisha na njia mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya jamii bado vinaokena kuwa vidogo. Asilimia sitini na mbili (62%) ya sampuli ya wahojiwa wetu wakati wa utafiti wa awali walikuwa wakitegemea njia moja tu ya kupata kipato kwa miezi 12 iliyopita na 21% walitegemea angalau njia mbili tu. Tofauti za kijinsia katika idadi ya vyanzo vya mapato ya fedha hazikuwa wazi, na kaya nne, zote zinazoongozwa na wanaume, ziliripoti kuwa hawana chanzo chochote cha kipato.

Takribani 77% ya sampuli ya wahojiwa waliripoti kuwa wanafuga mifugo kama chanzo chao kikuu cha kipato kwa mieze 12 iliyopita, na 50% ya kaya zinazoongozwa na wanawake wako kwenye kundi hili. Tofauti katika kilimo ni kwamba wakati 29% ya kaya zinazoongozwa na wanawake waliripoti kuwa kilimo cha mazao ndiyo chanzo chao kikuu cha kipato, ni 7% tu ya kaya zinazoongozwa na wanaume ndizo zilizoripoti kuwa kilimo ni chanzo muhimu cha kipato. Takwimu hizi zinaonesha kuwa wanawake wengi hawategemei mifugo kama chanzo cha kipato kwao ukilinganisha na kaya zinazoongozwa na wanaume, ambapo inaonesha kwamba huenda wanawake walifanikiwa kutokana na kutumia fursa hiyo ya kutofuga kufanya shughuli nyingine mbadala au kutokana na kile kinachodhaniwa kuwa wanawake walilazimika kujishughulisha na kazi nyingine za kujipatia kipato kutokana na ugumu wa kumiliki ardhi na mifugo suala ambalo ni tofauti sana kwa wanaume.

Ni 3% tu ya sampuli ya kaya zilizohojiwa ziliripoti kujihusisha na shughuli za uchimbaji ndani ya miezi 12 iliyopita kama chanzo chao cha kipato, na wote walikua wanaume. Kuna kaya mbili za ziada zinazoongozwa na wanawake zilizohojiwa na kutaarifu kuwa shughuli za madini ni chanzo chao kikuu cha kipato, na kaya ya tatu iliripoti kufanya biashara ya madini. Ingawa taarifa za kujihusisha kwenye shughuli za madini hazikuripotiwa vizuri kama chanzo kikuu cha kipato, watu wengi kwenye mahojiano na makundi ya watu binafsi walisema kuwa watu wengi ni wachimbaji wadogo, wafanyabiashara ya madini, na kukusanya madini kutoka kwenye mabaki ya udongo kazi ambayo hufanywa zaidi na wajane. Madini bila shaka yanachangia kipato kwa watu wa Naisinyai lakini pia yanachangia matatizo makubwa mno.

Ufugaji/kuchunga

Asilimia tisini na tatu (93%) ya kaya kutoka kwenye sampuli ya wahojiwa wakati wa utafiti wa awali zinaonesha kuwa jamii ilikuwa inatumia mifugo yao na wanyama wengine kwa ajili ya chakula/kuishi, ikilinganishwa na 41% tu ambao walisema kuwa walikuwa wakiuza wanyama wao hai. Kuwa na mifugo ni suala lenye umuhimu mkubwa kitamaduni kwa wafugaji wa Kimasai wa kijiji cha Naisinyai, na mifugo pia inatumika kama utajiri wa jadi/kimila na kama heshima kubwa pamoja na kulipia mahari. Watu wengi walikuwa wakiuza mifugo yao wakati unapohitajika na wakati wa ukame au shida, na siyo kwa ajili ya kupata fedha. Kinyume na hapo, ikiwa fedha inaweza kupatikana kutokana na vyanzo vingine, kama vile madini au kilimo, mifugo haitauzwa.

Kunaonekana kuwepo kwa utaratibu na msimamo wa mgawanyo wa kazi kijinsia, wanawake wanahusika zaidi kukamua, kuwatunza mifugo dhaifu/wagonjwa wakati wanaume wao kwa ujumla wanawajibika kunywesha mifugo, kuhamisha na kuuza mifugo. Ilikuwa ni nadra sana kwa wanawake kushiriki kuchinja mifugo na ilionekana kuwa katika kaya nyingi zinazoongozwa na wanawake hawakuwa wanauza mifugo badala yake shughuli hiyo ilifanywa na vijana/watoto wa kiume au ndugu wa mkuu wa kaya.

Kinyume chake, wanawake waliripotiwa kuwa wanahusika zaidi siku hizi katika ufugaji kuliko zamani, kwa sababu mbili. Kwanza, tangu kuanzishwa kwa elimu ya UPE watoto wengi waliandikishwa shuleni, na kuwafanya kutoweza kuendelea kufuga mifugo kutokana na kutumia muda mwingi shuleni. Pili, kadiri kijiji kinavyokuwa, wanaume wengi wamekuwa na shughuli nyingi na ikiwa ni pamoja na kilimo, na hivyo kuacha kazi za kila siku mikononi mwa wanawake. Licha ya hili,

majukumu ya mila na desturi kuhusiana na mifugo bado suala liko wazi kuwa iko kwenye mamlaka ya wanaume.

Kilimo cha Mazao

Asilimia themanini na mbili (82%) ya kaya za sampuli ya watu waliohojiwa wakati wa utafiti wa awali, zinaonyesha kuwa jamii ilikuwa ikifanya kilimo cha mazao, na kwenye wastani wa eneo la shamba lenye hekari 4.5. Zao kuu ni mahindi na maharage ni kidogo sana na kaya chache walikuwa wakiotesha alizeti, vitunguu na choroko.

Matumizi ya kawaida ya mazao yalikuwa ni kwa ajili ya chakula, lakini angalau aslimia tano ya mazao hayo yaliuzwa kwa kiasi cha gunia la mahindi na maharage kwa ajili ya kupata fedha katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kilimo cha mazao kwa ajili ya chakula na biashara/fedha kililingana kwa idadi kwenye kaya zinazoongozwa na wanaume na zile zinazoongozwa na wanawake. Lakini baadhi ya kaya zinazoongozwa na wanaume hazikuwa zikijihususha kabisa na suala la kilimo cha mazao.

Kilimo kwa kiasi kikubwa ni cha biashara, na wakulima wengi wanakodisha matrekta ili kuandaa mashamba yao; baadhi ya wakulima wa wanaume matajiri pia walielezea kuajiri vibarua wa kawaida ili kusaidia kuweka mbegu na kupalilia. Hii inaonyesha kwamba kunaweza kuwa na vikwazo kwenye kaya masikini zinazoongozwa na wanawake katika kujihusisha na kilimo cha mazao wanayoweza kumiliki na kupangia matumizi wenyewe isipokuwa mazao kidogo yatokanayo na bustani ndogondogo. Kaya hizi zinazoongozwa na wanawake watalazimika kutegemea nguvu kazi ya familia au kuajiri wafanyikazi/vibarua au matrekta kulingana na uwezo wao wa kiuchumi.

Wanaume waliripotiwa kushiriki katika kilimo cha jumla cha mazao kwa ajili ya chakula kwa asilimia 70 ya kaya zote zilizotokana na sampuli ya wahojiwa, ikilinganishwa na asilimia 37 tu ambapo wanawake walihusika. Katika kujadiliana kuhusu majukumu ya wanawake na wanaume katika kilimo, baadhi ya wanawake walidai kuwa wanaume wanajihusisha tu wakati wa kuvuna mazao ili kufahamu kiasi cha mavuno. Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa wahojiwa wengi katika makundi na watu binafsi, wakati wanawake walioolewa walikuwa wakilima kwenye mashamba waliyopewa na waume zao, wanawake wote kwa kawaida wanasaidiana na waume zao kwenye kilimo katika ardhi ya jumla ya kaya. Wanawake walionekana kushiriki zaidi katika kufanya kazi kama vile kupanda, kupalilia na kuvuna, na watu kutoka kwenye kaya zingine pia walishiriki kwa kuchangia fedha na kutoa ushauri.

Mahusiano ya kijinsia

Mgawanyo wa majukumu kijinsia unazingatia mila na desturi za Kimasai, wanawake wakihusika zaidi kwenye shughuli za nyumbani, ikiwa ni pamoja na kwenda kuchota maji pamoja na kukusanya kuni. Wanaume wana jukumu la kutoa mwongozo wa kazi/shughuli kwa mke/wake zake na watoto na kugawa majukumu mengine kwa watu wote wa kaya kadri aonavyo inafaa.

Ingawa wahojiwa wetu wengi kwenye makundi na watu binafsi walifikiri mgawanyo wa majukumu kijinsia yamebadilika kwa siku za hivi karibuni kwamba wanawake sasa wanajihusisha na shughuli za kujipatia kipato, ila bado matumizi ya fedha hiyo inaamuliwa na waume zao. Ni kiasi kidogo tu cha fedha kama vile inayotokana kwa kuuza maziwa inaamuliwa na wanawake na ilitumika kwa ajili ya famila tu na siyo kwa ajili ya matumizi binafsi ya mke/wake wenyewe. Kwenye kaya 54 zinazoongozwa na wanaume kutoka kwenye sampuli ya wahojiwa inayojumuisha mume na mke/wake, hakuna mwanamke aliyekuwa na kipato cha fedha kabisa, hali inayowafanya wawe tegemezi sana kwa waume zao na kukosa nguvu ya kupatania matumizi ya fedha inayotegemewa katika kuchangia uchumi wa kaya. Hata hivyo, baadhi ya wahojiwa katika makundi (na hasa wale wenye ndoa ya mke mmoja) waliripoti kuwa maamuzi ya matumizi ya fedha inafanyika kwa ushirikiano/pamoja.

Wanawake wengi waliripoti kuwa kukosa umiliki wa rasilimali na fedha ni tatizo na kikwako kikubwa cha maendeleo kwao. Tatizo jingine ni ukosefu wa elimu kwa wanawake na kukosa uwakilishi

kwenye uongozi, usimamizi na maamuzi ya masuala ya ardhi na maliasili. Jambo zuri ni kuanzishwa kwa vikundi 15 vya kuweka na kukopa vya wanawake huko Naisinyai ili wanawake waweze kusaidiana kuanzisha biashra ndogondogo. Wanawake pia walibuni njia ya kuhakikisha kuwa wanabaki na kufanya maamuzi juu ya fedha wanayopata kutokana na kujishughulisha kutafuta kipato ambayo ni kuweka fedha kwenye simu.

Uchimbaji wa Madini Naisinyai

Uchimbaji katika eneo la Mirerani umeongezeka kwa kiasi kikubwa tangu kugundulika kwa Tanzanite mwaka 1967, awali ikiwa ni uchimbaji mdogo na baadaye makampuni makubwa kuingia baada ya kuanzishwa rasmi kwa eneo tengefu la Mirerani mwaka 1995/96. Wakati wa utafiti wetu wa awali na awamu ya utafiti shirikishi kampuni kubwa pekee iliyokuwa inafanya kazi ni Tanzanite One na kampuni ya uchimbaji wa kati ilikuwa ni Tanzanite Afrika. Kampuni ya pili ya kati, Kilimanjaro Mining, ilianza kufanya kazi tena wakati tulipokuwa tunafanya kazi ya mrejesho kwa jamii ya Naisinyai mwezi wa saba na wa nane 2017, wakati ripoti ilipokuwa inaandikwa, lakini haikutajwa mara kwa mara wakati wa mahojiano na makundi lengwa na watu binafsi.

Kampuni ya Tanzanite One na Tanzanite Africa

Wamiliki wa kipindi cha nyuma wa Tanzanite One na mameneja walikuwa wameiacha kampuni kutokana na madeni makubwa mwaka 2014 lakini waliripotiwa kuwa na ujirani mwema na mahusiano mazuri sana na jamii. Kwa upande mwingine, wasiwasi mkubwa ulielezwa juu ya usimamizi mpya tangu wakati huo. Wahojiwa wengi waliripoti kuwa kampuni hiyo haijawahi kuajiri watu wa eneo husika/hilo na haina mahusiano mazuri na jamii. Kutokana na mabadiliko hayo, wanakijiji waliandamana wakidai huduma mbalimbali kutoka kwenye kampuni, na baadhi ya mabadiliko madogo yalifanyiwa kazi, kama vile kuwapa kikundi cha wakina mama mifuko yenye mabaki ya madini kutoka kwenye kampuni. Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzanite One alikiri kwetu (mwezi wa saba 2017) kwamba, ingawa kwa ujumla anafurahihswa na huduma za kampuni kwa jamii (CSR), kuna misaada zaidi inayoweza kutolewa kwa jamii. Alizidi kusema kuwa ingawa Afisa Mahusiano wa kampuni ana mahusiano mazuri na mwenyekiti wa kijiji na kwamba wanawasiliana mara kwa mara, mawasiliano zaidi yanahitajika hasa kupitia mikutano ya jamii.

Kampuni ya Tanzanite Africa pia inaonekana kutosaidia jamii vizuri na ni kwa nadra sana inaajiri watu wa jamii husika. Ingawa iliripotiwa kujenga kisima cha maji kwa ajili ya mifugo, bado wasiwasi ulibaki kuwa wachungi wanashindwa kufikia maeneo ya malisho kutokana na shughuli za kampuni na pia kampuni hii haikuwa ikiruhusu wanawake kuingia kwenye eneo la kampuni kukusanya mabaki ya madini kutoka kwenye mchanga. Kwa Tanzanite One, tulijifunza kuwa jamii haikubaliani na suala hili pia kutokana na kile kilochoelezwa kuwa jamii ilifanya maandamano kadhaa dhidi ya kampuni hiyo na mojawapo ya maandamano yalikuwa yakiongozwa na wanawake.

Wachimbaji wadogo

Wahojiwa wa makundi lengwa na watu binafsi wanaona kuwa leseni nyingi za wachimbaji wadogo ziko mikononi mwa watu wa nje na siyo wazawa. Wakati wanawake wachache wanamiliki leseni za awali (PMLs), ilionekana kuwa hakuna hata mwanawake mmoja wa Kimasai wa eneo hilo aliyekuwa na leseni. Kulikuwa na wasiwasi mkubwa juu ya ukosefu wa uwazi na uwajibikaji kuhusiana na wachimbaji wadogo, na mtazamo wa jumla wa ukosefu wa nguvu kwa serikali ya kijiji kulinda na kutetea haki za watu. Viongozi wa vijiji wenyewe wanaona kuwa sheria haiwapendelei wanakijiji na badala yake inalinda zaidi wachimbaji wadogo. Kwa upande mwingine, viongozi wa kijiji pia wanashukuru kuwa baadhi ya makampuni ya wachimbaji wadogo yamesaidia michango ya kifedha kwa jamii, kwa mfano walichangia fedha kwa ajili ya kujenga matundu ya vyoo vya shule.

Mchango wa uchimbaji madini kwa ustawi wa jamii

Kwa mujibu wa wahojiwa wengi wanawake katika makundi na watu binafsi, faida kubwa kutokana na madini huko Naisinyai imeelekea kwa wanaume. Wakati wanawake, na hasa wajane, wanakusanya madini kutokana na mabakai ya mchanga, hii ilikuwa ni shughuli hatari iliyosababisha unyanyasaji kwa wanawake ikihusisha matusi na kubakwa. Kwa upande mwingine, biashara ya madini, ambayo ilionekana kutoa fursa kubwa ya kupata kipato lakini fursa hizo zilikuwa mikononi mwa wanaume, na hata fursa nyingi za ajira ziliwalenga wanaume na siyo wanawake. Hata hivyo, baadhi ya miundombinu ya ndani ilijengwa na makampuni ya madini, ikiwa ni pamoja na visima na mabomba ya maji, na baadhi ya majengo yalifanyiwa ukarabati; aina hii ya faida zisizo za moja kwa moja zinaonekana kuwagusa/kuwanufaisha wanawake na wanaume, hutokana na madini. Kwa nyongeza, uchimbaji madini imechangia maendeleo huko Naisinyai kwa ujumla, uwepo wa masoko ya chakula, kuwepo kwa maduka mapya na ujenzi wa barabara ya lami kutoka Naisinyai hadi uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro.

Kazi

Makampuni makubwa yanayofanya kazi ndani ya eneo tengefu la Mirerani (MCA), pamoja na makampuni ya wachimbaji wadogo hayaajiri watu wa jamii/eneo hilo. Tuliambiwa kuwa kazi wanazopewa wazawa ni za ulinzi na ilikuwa kwa ajili ya wanaume tu ambapo hata hivyo kazi hizo hazipatikani kirahisi. Kulingana na taarifa zilizotolewa na wahojiwa kwenye makundi na watu binafsi, vijana wa Naisinyai kama 200 waliajiriwa na wamiliki wa awali wa kampuni ya Tanzanite One, lakini karibu wote waliacha kazi na wazawa sita tu ndiwo waliobaki wakiwa wameajiriwa na kampuni hiyo. Wanaume hao wachache waliobaki kama wafanyakazi wa kampuni hizi ndani ya eneo tengefu la Mirerani waliripoti kufanya kazi katika mazingira magumu na mishahara midogo. Makampuni mengi ya wachimbaji wadogo hawakuwa na kazi za moja kwa moja, lakini badala yake walikuwa wakiruhusu wanaume kuchimba na kukusanya mabaki ya madini kutoka kwenye mchanga.

Kukusanya na kufanya biashara ya madini

Kutokana na ukosefu wa fursa za ajira kwenye makampuni ya madini wanaume wengi wamejikita katika biashara ya udalali wa madini, kununua mabaki ya madini kutoka migodini na kuuza kwa soko kubwa la madini ya Tanzanite kwenye mji mdogo wa Mirerani. Ingawa wengi wa wafanyabiashara na madalali hawa ni wanaume, baadhi ya wanawake pia wanahusika. Kuna ishara zinazoonekana wazi kwamba baadhi ya wanaume wametajirika kutokana na shughuli hii, lakini ilikuwa ni vigumu kufahamu kiasi cha uchimbaji na biashara ya madini imetengeneza fursa ya utajiri kwa watu wengi zaidi kiasi gani, kutokana na kile kilichoelezwa na wale wenye leseni kuwa ni vigumu kupata faida kubwa kutokana na gharama za uendehsaji.

Kama ilivyoonekana hapo juu, kukusanya na kuokota mabaki ya madini kutoka kwenye mchanga imetoa fursa kwa wanawake masikini na haasa wajane kujipatia kipato cha fedha inayowasaidia kuweza kununua chakula kwa ajili ya familia zao. Hata hivyo, kuna matatizo mengi kwa wanawake katika hili. Wanatembea saa nne kwenda migodini na hawaruhusiwi kuingia migodini na kuokota madini. Kuna nyakati wanatukanwa, wanapigwa na kubakwa na takribani watu wanne wameuwawa na wanaume wasioajiriwa waliokuwa wakisubiri pia kukusanya mabaki ya madini kutoka kwenye mchanga. Wahojiwa wetu kwenye makundi na watu binafsi waliripoti kuwa wanawake huenda migodini kama kundi au kwa kusindikizwa na wanaume, lakini bado walithalilishwa na kuwa kwenye mazingira hatarishi. Tuliambiwa kuwa wanawake wengi waliowahi kubakwa wakiwa kwenye ndoa, walithalilishwa zaidi hata na waume zao, kwa kuwalaumu juu ya kubakwa. Pia kuna unyanyapaa mkubwa katika suala la kubakwa na hivyo wanawake wengi hawakutaka kuweka wazi kitendo hicho na waume zao walifahamu tu endapo ubakaji umesababisha ujauzito. Ingawa viongozi wa kijiji wanafahamu suala hili ndani ya jamii, wanawake wengi tuliozungumza nao walisema kuwa hakuna jitihada madhubuti zinazofanyika kuwalinda.

Athari za Uchimbaji Madini

Wakati makampuni ya madini Naisinyai (hasa Tanzanite One) yalionekana kuiletea faida jamii, faida kwa jamii kutoka kwa wachimbaji wadogo haionekani moja kwa moja badala yake wanaonekana kusababisha matatizo makubwa ya kijamii yaliyoathiri hasa wanawake. Wachimbaji wakubwa na wadogo wanaonekana kutoa fursa ya kusaidia jamii kupata kipato cha fedha isiyo ya moja kwa moja kwa kuiruhusu jamii kuokota madini kutokana na mabaki ya mchanga. Hata hivyo, utafiti wetu ilibaini kuwa kuna malalamiko mengi yanayohusu wachimbaji wakubwa na wadogo, ikiwa ni pamoja na kuchukua na kuharibu maeneo ya malisho, kuharibu ubora wa rasilimali za maji, na zaidi sana kubakwa na kuuwawa kwa wanawake na watoto.

Wakati watu wengine wanalalamikia serikali ya kijiji kwa kutolinda haki za jamii, kwa mfano kwa kuwahimiza wanakijiji kuacha kuyapinga makampuni makubwa ya madini, wengine waliona kwamba serikali ya kijiji haina nguvu ya kupingana na makampuni makubwa na wachimbaji wadogo walioko kwa kuwa walipewa maeneo kisheria. Pia kulikuwa na hofu kwamba ardhi zaidi katika eneo hilo itatengwa kwa ajili ya uchimbaji madini kutokana na utafiti wa kisayansi uliofanyika hivi karibuni.

Uharibufu wa Mazingira

Ingawa matokeo ya kijamii yatokanayo na madini yalionekana wazi zaidi kuwakandamiza wanawake huko Naisinyai, uharibufu wa mazingira unaonekana kumwathiri kila mtu. Kwa ujumla imeonekana kuwa kukuwa kwa uchimbaji wa madini na kuongezeka kwa idadi ya watu imepunguza uoto wa misitu na eneo la malisho ndani ya kijiji. Aidha, makampuni makubwa na wachimbaji wadogo wa madini waliripotiwa kuchimba mashimo mengi katika ardhi, na mara nyingi yaliachwa wazi na kubaki kama tishio kwa wanadamu na mifugo, hasa kwa kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo ambako hakuna uzio. Watu wengine tuliozungumza nao pia walitaja ongezeko la jumla la uchafuzi wa mazingira, kama vile uchafu wa madini unamwagwa kwenye ardhi ya malisho.

Masuala maalum yalitolewa juu ya kemikali zinazotumiwa katika usafishaji wa madini ya Tanzanite na kutomwaga mahali maalum, hasa karibu na makazi ya binadamu. Inahusishwa na suala zima la kupungua kwa ubora wa maji, huku baadhi ya watu pia wakidhani kwamba kumekuwepo na idadi kubwa ya upasuaji kwa watoto na wanawake wazee wenye miguu iliyopinda kwa sababu ya kemikali zinazotumiwa na makampuni ya madini ndani ya eneo tengefu la Mirerani.

Mchakato/utaratibu wa kupata ardhi

Usimamizi wa ardhi na mtazamo wa sheria

Kabla ya uanzishwaji wa vijiji, ardhi ya Naisinyai ilikuwa ikisimamiwa kwa utaratibu wa kimila na baadaye kutolewa kama urithi kwa ndugu wa familia na ukoo. Hata hivyo, usimamizi wa kisheria umeonekana kupata nguvu zaidi. Yeyote aliyehitaji ardhi kwa aijili ya kilimo na makazi alipaswa kuomba kwa kupitia serikali ya kijiji au kuipata ardhi hiyo kwa kununua ingawa ardhi ya malisho bado inaonekana kusimimiwa kwa utaratibu wa mila na desturi.

Serikali ya kijiji na Ilaigwanak kwa pamoja, ni mabaraza yanayoongozwa zaidi na wanaume na wanawake hawaonekani wakishiriki sana kwenye usimamizi na ulinzi wa ardhi na maliasili nje na wajumbe walioko kwenye serikali ya kijiji kisheria (kwenye taasisi za kiserikali).

Wakati washiriki wengi kwenye makundi na watu binafsi waliohojiwa walidai kuwa tayari wanawake wanayo haki sawa na wanaume juu ya umiliki na usimamizi wa ardhi au wanawake hawahitaji kumiliki ardhi wengi hawafahamu hazi zao za kisheria. Hata mahali ambapo wanawake wanafahamu sheria, inaonekana kuwa mila na desturi zinawakwamisha kudai haki zao. Zaidi ya hayo, hata pale ambapo wanaume wanafahamu usawa wa kijinsia kwenye sheria ya Tanzania, uelewa huu haujasaidia kupunguza msimamo wao kuwa wanawake hawahitaji/ hawana haja ya kudai haki ya kumiliki ardhi, wanawake wengi wanafahamu kuwa hawatendewi haki na hivyo wanatamani kuona

mabadiliko kuhusu haki za ardhi; hata hivyo, kwa kuwa aina yeyote ya ardhi wanayoitaka wanawake watapata kwa waume zao na au ndugu wengine wa kiume.

Upataikanaji wa ardhi kwa ajili ya makazi na kilimo

Wakati wa utafiti wetu, Kijiji cha Naisinyai hapakuwa na Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi unaosaidia kusimamia na kulinda ardhi ya kijiji. Imeonekana kuwa upatikanaji wa ardhi umekuwa mgumu kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na ufinyu wa ardhi. Kipindi cha nyuma watu waliweza kujipatia kiasi chochote cha ardhi waliyohitaji kwa ajili ya kilimo na makazi, wakati huu kila mtu anatakiwa kununua ardhi au kuomba (kiasi kidogo cha ardhi kilichopo) kwa kupitia serikali ya kijiji kwa kulipia, na hivyo hali hii kufanya upatikanaji wa ardhi kuwa mgumu hasa kwa watu masikini.

Mchakato wa kuomba ardhi kwenye serikali ya kijiji ni sawa kwa ardhi ya kilimo na makazi. Lakini imeonekana kwamba ardhi kwa ajili ya kilimo hakuna tena na hivyo namna pekee ya kupata ardhi siku hizi ni kwa kurithi au kukodisha au kununua kutoka kwa wamiliki wengine; njia mbadala nikwenda kutafua ardhi ya kilimo kwenye vijiji vya jirani. Mara nyingi watoto wa kiume wanarithi lakini mara chache pia wajane wanarithi mashamba, na katika ndoa za wake wengi sehemu ya ardhi ya urithi inatumika na wake wengine kama ardhi ya makazi. Haki za wanawake katika ardhi hii ya urithi hailindwi, hata hivyo, baadhi ya ndugu na majarani wanawanyang'anya kwa nguvu ardhi hiyo.

Ingawa watu wengi hawana hati yoyote ya ardhi yao, bado wanajisikia kuwa wana uhakika wa umiliki. Hata hivyo, wengi wanatambua kuwa bila hati ya umiliki haki za ardhi hazina usalama, hivyo wangependa kuwa na hati miliki ya ardhi kisheria au haki zao za kimila za umiliki zilindwe.

Migogoro ya Ardhi

Ilikuwa wazi kuwa watu wengi wa Naisinyai wanatazama migogoro ya ardhi na maliasili zingine kuwa ni tatizo kubwa, ikiwa na pamoja na migogoro na makampuni ya uchimbaji, wachimbaji wadogo na jamii. Pia suala la upatikanaji wa haki, wanaume na wanawake wengi waliona kuwa ni vigumu kupata haki stahiki kwenye migogoro inayohusiana na ardhi na malisili huko Naisinyai.

Migogoro ya mipaka ya mashamba iliripotiwa kuwa mingi kutokana na kilichoelezwa kuwa mipaka yenyewe haikuwa wazi/haieleweki vizuri. Kwa sababu hii, Baraza la Ardhi la Naisinyai huitisha vikao katika msimu wa masika ili kujadili na kutafuta suluhu juu ya migogoro ya ardhi kati ya wanakijiji. Endapo migogoro hii haitasuluhushwa vizuri na Baraza la Ardhi basi hupelekwa kwa Ilaigwanak.

Upataikanaji wa ardhi kwa wanawake kupitia utaratibu wa kisheria

Ingawa utaratibu wa kisheria na soko la ugawaji wa ardhi huko Naisinyai unatoa fursa sawa kwa wanaume na wanawake kumiliki ardhi, inaonekana kuwa kiuhalisia kuna vikwazo/changamoto za kimuundo ikijumuisha mila na desturi potofu zinazowakwamisha wanawake wasipate ardhi kupitia utaratibu wa kisheri. Tulijifunza kuwa wanawake walioolewa wataomba tu ardhi ya kulima kwa waume zao na siyo kwenye serikali ya kijiji (hata kama ardhi ya kupewa ingekuwepo); hata wanawake (wajane) hawezi kuomba ardhi kwa ajili ya makazi weneywe. Kutokana na uhaba mkubwa wa ardhi, suala la ukosefu wa rasilimali fedha kwa wanawake limetajwa kuwa ni tatizo kubwa sana inayokwamisha wanawake kupata ardhi.

Usimamizi wa Ardhi ya Malisho/kuguga

Hali ya ufugaji huko Naisinyai imebadilika kwa kiasi kikubwa tangu miaka ya 1960, na hasa zaidi miaka kumi iliyopita, sio tu kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi lakini pia kuongezeka kwa idadi ya watu, pamoja na kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji madini ambaypo kwa kiasi kikubwa inaonekana kuchukuwa sehemu kubwa ya ardhi ya malisho ya kijiji, na sehemu kubwa pia ya makazi ya watu. Kwa hiyo, umbali wa malisho uliongezeka, kwa sababu hiyo watu wengi walisema kwamba mifugo yao sasa inachungwa na majirani au wafanyakazi walioajiriwa

wanaotoka nje ya kijiji kwa muda mrefu au mwaka mzima. Hata hivyo, licha ya changamoto ya rasilimali ardhi ya malisho na matatizo mengi kwa wachungi, ufugaji bado ni kipaumbele cha wengi kama namna ya kujipatia kipato cha fedha, kwa kuwa wanaweza kupata fedha kutokana kuuza mifugo kwa mwaka mzima na ilionekana kuwa ni namna ya kuaminika kuliko kilimo cha mazao.

Upataikanaji wa maeneo ya malisho na kubadilika kwa mwelekeo wa kuhama

Idadi kubwa ya kaya zilizohojiwa kwenye utafiti wa awali ziliripoti kuomba mifugo yao ichungwe na majirani/kaya nyingine, na kaya zinazoongozwa na wanaume walionekana kutumia mfumo huu wa ufugaji zaidi ikilinganishwa na kaya zinazoongozwa na wanawake. Mifugo mingi ya kaya zinazoongozwa na wanawake walionekana kuchunga mifugo yao wenyewe kwa kuwa hawana mtu mwingi wa kuchunga (hakuna wanaume kwenye kaya zao) au pia kwasababu hawawezi kuwalipa wafanyakazi wa kufuga.

Kaya nyingi za Naisinyai huwatuma watoto wao wakubwa wa kiume kuhamisha mifugo au kuwalipa watu waweze kuhamisha mifugo yao; Kwa ujumla kaya zenye utajiri mkubwa wa ng'ombe wengi wanategemea zaidi watu wanaolipwa kuhamisha mifugo yao wakati kaya zenye mifugo michache wanawategemea wanafamilia kufanya hivyo. Mzunguko, umbali na urefu wa maeneo ya kuhamia kutafuta/kufuatilia malisho yanaonekana kuongezeka katika miongo miwili iliyopita. Wale ambao walikuwa wakichunga mifugo yao kwa umbali wa kilomita 20 hadi 30 kutoka maeneo yao ya makazi waliweza kuwaleta mifugo yao kunywesha kila baada ya siku chache, lakini wale waliohamisha mifugo yao takribani kilomita 100 wanahama wakati wa ukame bila kurudi kwa miezi mingi mpaka mvua nyingi zinyeshe kati ya Machi na Juni.

Ni sehemu kidogo sana ya ardhi kwa ajili ya malisho ndiyo iliyobaki ndani ya kijiji cha Naisinyai na linatumiwa na watu wachache sana, hasa wanawake na watoto wadogo wanaohitaji maziwa mara kwa mara hivyo wanalazimika kuwa na ng'ombe karibu. Wanawake hao waliruhusiwa kupitisha mifugo yao katikati ya maeneo ya uchimbaji wa madini ili kufikia eneo hilo la malisho, lakini ilikuwa ni hatari sana kupitisha mifigo maeneo ya uchimbaji madini kutokana na mashimo yaliyo wazi ambapo mifugo wanaweza kutumbukia na hatari kubwa iliyotajwa awali juu ya kubakwa au kunyanyaswa kwa wanawake katika maeneo yaliyozunguka migodi.

Changamoto nyingine inayowakumba wafugaji wa Naisinyai ni ukosefu wa mvua kwa miaka ya hivi karibuni, kukauka kwa mito na matokeo hasi inayosababishwa na mashamba makubwa ya umwagiliaji na uchimbaji madini. Hakuna mifugo inayotoka jirani nakuhamia Naisinyai, ila baadhi ya watu binafsi kutoka ndani ya Naisinyai wanaomba kuchunga mifugo yao kuchungwa kwenye mashamba baada ya kuvuna.

Hitimisho

Kijiji cha Naisinyai kimebadilika kwa haraka katika miongo michache iliyopita. Kama mahali pekee duniani ambako madini ya Tanzanite yanapatikana, uchimbaji wa madini hayo umeongezeka kwa kiasi kikubwa katika eneo la Mirerani tangu uchumi wa uchimbaji wa madini Tanzania ulipoanza kukuwa kwa kasi miaka ya 1990. Matokeo yake, maeneo yenye uoto na malisho yamefyekwa kwa ajili ya uchimbaji wa madini yenyewe na kwa ajili ya upanuzi wa makazi, mashamba na miundombinu.

Uchimbaji madini umechangia kwa ufanisi mkubwa maendeleo ya kiuchumi na miundombinu ya eneo hilo na baadhi ya watu wamepata utajiri mkubwa kutokana na madini ya Tanzanite. Hata hivyo, pia imebadilisha hali ya ufugaji wa ndani, kama vile wafugaji hivi sasa wanalazimika kuhamia mbali zaidi kufuata malisho na watu wengi huko Naisinyai wanalazimika kupeleka mifugo yao vijiji vya jirani kwa mwaka mzima mifugo yao katika vijiji vingine vya mbali. Pia kumekuwepo na matokeo hasi ya kijamii na ya mazingira yaliyosababishwa na uchimbaji wa madini kwa jamii ya Naisinyai, ambapo matukio mengi yalionekana kuwanyanyasa wanawake.

Wakati majukumu ya kijinsia yalionekana kubadilika polepole sana, wanawake hivi sasa wanazidi kujihusisha katika ufugaji na shughuli za kuzalisha kipato, bado wanawake hawakuwa wakimiliki ardhi, mifugo wala mali nyingine na mara nyingi walilazimika kukabidhi fedha yoyote wanayopata kwa waume zao.

Wakati huohuo, unyanyasaji unaotokana na madini umeongezeka, ubakaji na udhalilishaji umeongezeka hasa kwa wanawake, na kufanya kazi zao za kila siku, kama kukusanya kuni na kuchunga mifugo kuwa hatari zaidi. Pia, faida ndogo ambazo wanawake wanapata kutokana na kukusanya mabaki ya madini kwenye mchanga zinapelekea wanawake kuacha shuguli hiyo kuliko hatari zinazo ambatana. Wakati serikali ya kijiji inafahamu matatizo haya, kwa kiasi kikubwa imeonekana kuwa haina nguvu na wakati huohuo wanawake wengi walidhani kuwa jamii inayoongozwa na wanaume inahitaji kufanya jitihada zaidi kuwalinda wanawake.

Vikundi kadhaa vya wanawake vinatoa fursa kwa wanawake kupaza sauti zao kwa pamoja na kuzalisha kipato cha fedha, na mabadiliko zaidi kama haya yanaweza kuwasaidia watu wa Naisinyai na kusaidia maendeleo endelevu ya kijiji. Wakati huohuo wakati wa utafiti wetu ilionekana wazi kuwa makampuni ya madini na wachimbaji binafsi wanahitaji kufanya kazi kwa pamoja na jamii nzima kutengeneza fursa zaidi kwa wanawake na watu wanaoishi katika mazingira magumu na kwa pamoja kuwatia nguvuni wachocheaji wa matendo ya unyanyasaji kwa wanawake.

mokoro

HakiMadini